



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 23 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

173. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa
Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ni jambo la kutia moyo kwamba maombi ya Passport
yanafanywa mtandaoni (*online*) kwa kujaza fomu na
kuwasilisha nyaraka zote husika mtandaoni. Kwa kuwa mifumo
ya NIDA na mifumo ya Uhamiaji imeungana na inaonana na kwa
vile NIDA huchukua alama za vidole (finger prints), picha na
taarifa nyengine.

- (a) Je, Serikali haioni kwamba hakuna ulazima wa Uhamiaji
kuomba tena nakala za nyaraka zote kwa njia ya karatasi
(hard copies).
- (b) Je, Serikali haioni kwamba hakuna ulazima wa kuchukua
tena alama za vidole kwa vile alama za vidole
zilizochukuliwa na NIDA ndizo zilizotumika kutengeneza
Kitambulisho cha Taifa ambacho ndio msingi mkuu wa
Utaifa.
- (c) Je, Serikali haioni kwamba mchakato huu mpya
wa Pasi ya Kielektoniki (ePass) umeongeza zaidi ukiritimba
kuliko kuuondoa.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

178. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Katika kuhakikisha kwamba Zanzibar inaondokana na vitendo viovu vyta ubakaji, Serikali kwa nia njema iliweka Sheria inayohusiana na ubakaji. Hata hivyo, Sheria hiyo inakaribisha urasimu katika kuitekeleza pindi wakihusika watu wasio na nia njema.

- (a) Je, katika ulimwengu mpya wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, Serikali ina mpango gani wa kuiboresha Sheria hiyo ili ipunguze urasimu katika kuitekeleza.
- (b) Je, ni kesi ngapi za ubakaji kwa mwaka 2021/2022 zimethibiti na kupatiwa hukumu na ngapi hazikuthibiti na kutolewa maamuzi.
- (c) Je, kwa wastani kesi ya ubakaji huchukua muda gani tokea kushikwa kwa mtuhumiwa hadi kupata hukumu au maamuzi.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

115. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Mazoezi ya viungo ya kila siku ni muhimu sana katika suala zima la kuweka mwili sawa na kunyoosha misuli pamoja na kuweka sawa chumvi pamoja na sukari katika mwili wa binadamu.

Kwa kuwa maeneo mengi katika miji tayari yamehamasika na mazoezi hayo hatimae kuanzisha vikundi mbali mbali kama 'KITAMBI NOMA' ambayo hufanya mazoezi kila siku asubuhi, na kwa kuwa wanavikundi hivyo wamefanikiwa kurekebisha mili yao sambamba na kurekebisha afya zao.

Je, ni lini Serikali kuititia Serikali za shehia zitahamasisha uanzishaji wa vikundi hivi pamoja na kutoa hamasa kwa mwananchi mmoja mmoja kwenye shehia na vitongoji.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

163. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa kuwa baadhi ya vijiji vya Fuoni Kibondeni (kwa Shaaban Ali) na Fuoni Bwiti zinapata umeme mdogo sana (hafifu).

Je, ni lini Shirika la Umeme litaondoa kasoro hiyo ya umeme hafifu katika vijiji hivyo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

101. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wananchi wa jimbo la Tumbe hususani wa vijiji vya Shumba Vyamboni, Gombe, Bule na Chimba kwa ujumla wamefurahi sana na kipongeza Serikali yao kwa kuingiza bajeti kwa ajili ya barabara yao ya Finya-Kicha.

- (a) Wananchi wanataka kujua, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utanza.
- (b) Je, kuna mpango gani wa kuwalipa fidia watakaoathirika.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

182. MHESHIMIWA SHADYA MOHAMED SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayochukuwa dhidi ya wafanyabiashara ambao hupandisha bei kiholela. Licha ya juhudi hizo bado tatizo la kupandisha bei bidhaa liko juu.

Je, Serikali ina mpango gani mbadala dhidi ya wafanyabiashara hao.

II. **HOJA ZA SERIKALI:**

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
23 Mei, 2022.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA